HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

MUHTASARI WA MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 12/02/2016

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1.	Mhe. Juma A. Kimisha	-	Diwani Kata ya Nyamilangano- **Mwenyekiti**
2.	" Gagi Lala Gagi	-	Diwani Kata ya Igwamanoni – **Makamu Mwenyekiti**
3.	" Tabu R. Katoto	-	Diwani Kata ya Igunda
4.	" Yohana M. Emmanuel	-	Diwani Kata ya Mapamba
5.	" Emmanuel N. Makashi	-	Diwani Kata ya Sabasabini
6.	" Mabala K. Mlolwa	-	Diwani Kata ya Chona
7.	" Yuda L. Majonjos	-	Diwani Kata ya Idahina
8.	" Mkomba P. Daudi	-	Diwani Kata ya Ukune
10.	" Kulwa D. Shoto	-	Diwani Kata ya Bukomela
11.	" Bundala J. Christopher	-	Diwani Kata ya Uyogo
12.	" Benedicto A. Mabuga	-	Diwani Kata ya Mpunze
13.	" Pili E. Sonje	-	Diwani Kata ya Ushetu
14.	" Sharifu A. Samwel	-	Diwani Kata ya Kinamapula
15.	" Paschal N. Mayengo	-	Diwani Kata ya Ulowa
16.	" Doa M. Limbu	-	Diwani Kata ya Nyankende
17.	" Kulwa E. Mabula	-	Diwani Kata ya Ulewe
18.	" Damas J. Njige	-	Diwani Kata ya Chambo
19.	" Hamis M. Majogoro	-	Diwani Kata ya Ubagwe
20.	" Joseph M. Masaluta	-	Diwani Kata ya Bulungwa
21.	" Golani P. Sayi	-	Diwani Kata ya Kisuke
22.	" Bernadetha M. Jumanne	-	Diwani Viti Maalum
23.	" Mary I. Lundalila	-	Diwani Viti Maalum
24.	" Bether M. Bugaywa	-	Diwani Viti Maalum
25.	" Esther M. Imambo	-	Diwani Viti Maalum
26.	" Felister N. Kabasa	-	Diwani Viti Maalum
27.	" Eva P. Mkonya	-	Diwani Viti Maalum
28.	" Gabriela A. Kimaro	-	Diwani Viti Maalum
29.	Ndg. Isabela O. Chilumba	-	Mkurugenzi Mtendaji (W) - **Katibu**

WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA

Mhe. Elias J. Kwandikwa - Mbunge Jimbo la Ushetu (kwa taarifa)

WATAALAM WALIOHUDHURIA

1.	Ndg.	Alfred Rukelegwa	- Kaimu Afisa Mipango (W)
2.	"	Benedicto Antony	- Kaimu Mweka Hazina (W)
3.	"	Christina Akyoo	- Kaimu Afisa Utumishi (W)
4.	"	Paschal Kalima	- Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)
5.	Dr.	John Duttu	- Kaimu Mganga Mkuu (W)
6.	Ndg.	Athanas Lucas	- Afisa Usafi na Mazingira (W)
7.	"	Gasati Silla	- Kaimu Afisa Biashara (W)
8.	"	Gervas Magogozwa	- Afisa Utamaduni (W)
9.	"	Marco Mwairwa	- Afisa Ardhi na Maliasili (W)
10.	"	Elias Macha	- Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
11.	"	Mkama Msilanga	- Kaimu Mhandisi wa Maji (W)
12.	Eng.	Bright Mndeme	- Mhandisi wa Ujenzi (W)
13.	Ndg.	Minael Ngomoi	- Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
14.	"	Melkiad Gaka	- Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
15.	"	Anna Ngongi	- Afisa Kilimo na Ushirika (W)
16.	"	Deogratias Rugangila	- Afisa Ushirika (W)
17.	"	Neuster James	- Mwanasheria (W)
18.	"	Godfrey Lwambura	- Fundi Sanifu
19.	"	Morgan Mwita	- Mratibu wa kudhibiti UKIMWI
20.	"	Jackson Wanyancha	- Kaimu Afisa TEHAMA (W)
21.	"	Nimilwa Lucas	- Kaimu Afisa Utumishi - TSD
22.	"	Willibard Samamba	- Kaimu Afisa Uchaguzi (W)
23.	"	Cosmas Maganga	- Mhasibu Mapato
24.	"	Juma R. Ngogo	- Afisa Mipango Miji
25.	"	Denis J. Pius	- Mratibu wa TASAF
26.	"	Thabiti Matepet	- Katibu Tawala (W)
27.	"	Phillipo Karol	- Mkaguzi wa Ndani (W)
28.	"	Mvano Karumbete	- Afisa Ugavi (W)
29.	"	Kawishe Lucas	- Afisa Ufugaji Nyuki (W)
30.	"	Salakana J. Peter	- Afisa Tarafa – Mweli
31.	"	Tumshukuru C. Mudui	- Afisa Tarafa - Dakama
32.	"	Ephraim Kaijuko	- Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Elimu Msingi (W) Kahama

WAGENI WALIOHUDHURIA

1.	Ndg.	Amos D. Ndege	- Afisa Uhamiaji
2.	"	Isani Lali Mjimbi	- Mkuu wa Magereza (W)
3.	"	Frank Elophacy	- Afisa Zimamoto (W)
4.	"	Mrisho Masoud	- Mshauri wa Mgambo (W)

5.	Ndg. Mayika Kisanjo	-	Kny: Mkuu wa Polisi (W)
6.	" John Sihali	-	Usalama wa Taifa (W)
7.	" Amina Mbwambo	-	Mwandishi wa habari - Kahama FM
8.	" Shaban Alley	-	Mwandishi wa habari - Star TV
9.	" Mkolla Kabali	-	Katibu UVCCM (W) Kahama
10.	" Shaban Njia	-	Mwandishi wa habari–Raia Tanzania
11.	" Simon Dionizy	-	Mwandishi wa habari–Radio Kwizera
12.	" Raymond Mihayo	-	Mwandishi wa habari – Habari Leo

SEKRETARIETI

1.	Ndg. Chamo Mashauri	-	Mwandishi wa vikao (CC)
2.	Ndg. Ashura Hoja	-	Mwandishi wa vikao (CC)

MUHT. NA. BM/34/2015/ 2016 – KUFUNGUA MKUTANO

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwakaribisha wajumbe, wataalamu, wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Wilaya, wageni waalikwa na wasikilizaji waliohudhuria mkutano huo. Alieleza kuwa madhumuni ya mkutano huo maalum ni kupokea, kujadili na kupitisha mapendekezo ya mpango wa bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Alieleza kuwa kwa kawaida haya ni mapendekezo ya mpango wa bajeti na baadaye bajeti kupitishwa na Bunge, ndipo tutapewa mrejesho wa bajeti halisi ya Halmashauri. Baada ya maelezo hayo Mkurugenzi Mtendaji (W) alimkaribisha mwenyekiti kufungua mkutano.

Mwenyekiti alisema kuwa mapendekezo hayo ya mpango wa bajeti yameshajadiliwa kwa kina katika vikao vya kamati mbalimbali za Halmashauri hivyo ana imani kuwa mjadala hautakuwa mrefu.
Mwenyekiti alifungua kikao saa 05:13 asubuhi.

MUHT. NA. BM/35/2015/2016 – KUPITIA NA KUJADILI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA BAJETI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU KWA MWAKA 2016/2017

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa hiyo. Alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu imekadiria kutumia jumla ya **Tshs 31,279,395,136.00** katika bajeti ya mwaka 2016/17 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.6 ukilinganisha bajeti ya mwaka 2015/2016 iliyokuwa Tshs 28,275,506,555.01

Alieleza kuwa bajeti ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2016/17 - 2018/2019 ni mpango ulioandaliwa kwa kutumia mfumo wa Medium Term Expenditure Framework (MTEF) kwa kutumia program ya PlanRep. Utaratibu huu unaelekeza matumizi ya fedha kutokana na malengo makuu 8 ya Halmashauri ya Ushetu na shughuli mahususi ambazo ziko bayana na imezingatia:-

1. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020
2. Dira ya maendeleo ya Taifa hadi 2025
3. Mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (5) awamu ya pili
4. Malengo ya maendeleo endelevu (SDGs)
5. Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)
6. Sheria, sera, miongozo, kanuni, nyaraka na maagizo ya serikali ya awamu ya 5
7. Vipaumbele vya wananchi kutokana na mipango shirikishi jamii (O & OD)
8. Sera za kijumla za Uchumi kama zilivyoelezwa katika miongozo ya uandaaji wa bajeti hii

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inakadiria kupokea na kukusanya kiasi cha Tshs **31,279,395,136.00** kwa ajili ya mishahara, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, ikiwa Tshs **28,962,102,936.00** ni ruzuku toka Serikali Kuu na wahisani mbalimbali ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na bajeti ya 2015/16. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la mishahara kwa watumishi wapya na kupandishwa vyeo.

Kwa mwaka wa fedha wa 2016/17, Halmashauri inakisia kukusanya Tshs **2,317,292,200** kutokana na makusanyo ya vyanzo vya mapato ya ndani sawa na ongezeko la asilimia 6.5 ukilinganisha na mwaka 2015/16 na hii imetokana na uboreshaji na ubunifu wa vyanzo vya mapato ya ndani.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alielezea vipaumbele kwa bajeti ya 2016/2017, kwa upande wa miradi ya maendeleo, bajeti hii imezingatia vipaumbele katika sekta ya elimu, maji, afya na miundombinu ya barabara hii ikiwa ni pamoja na kuchangia matengenezo ya madawati kwa shule za msingi na sekondari, ujenzi wa majengo ya utawala, nyumba za watumishi katika makao makuu (Nyamilangano) na ujenzi wa hospitali ya Wilaya Ushetu eneo la makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Ushetu.

Makisio ya bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa kila Idara na Vitengo

Na.	Idara/Kitengo	Bajeti iliyopitishwa 2015/2016 shilingi	Bajeti pendekezwa 2016/2017 shilingi
1.	Idara ya Elimu Msingi & Utamaduni	1,052,711,551.00	1,533,086,568.00
2.	Idara ya Elimu Sekondari	1,227,776,888.00	1,052,495,888.00
3.	Idara ya Afya	1,625,216000.00	1,150,216,000.00
4.	Idara ya Usafi na Mazingira	17,000,000.00	20,000,000.00
5.	Idara ya Maji	1,261,405,915.00	1,252,705,915.00
6.	Idara ya Maendeleo ya Jamii	112,893,099.00	85,142,360.00
7.	Idara ya Mipango na Takwimu	206,826,500.00	200,450,871.00
8.	Idara ya Kilimo na Ushirika	325,350,520.00	322,477,740.00
9.	Idara ya Mifugo na Uvuvi	59260,661.00	147,000,000.00
10.	Idara ya Ardhi na Maliasili	59,260,661.00	147,000,000.00
11.	Idara ya Ujenzi	684,210,000.00	1,698,138,000.00
12.	Kitengo cha Ufugaji Nyuki	17,000,000.00	17,000,000.00
13.	Idara ya Fedha na Biashara	150,000,000.00	117,000,000.00
14.	Idara ya Utawala na Utumishi	16,420,800,117.00	21,570,738,168.00
15.	Kitengo cha Sheria	17,000,000.00	19,000,000.00
16.	Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani	25,272,000.00	28,000,000.00
17.	Kitengo cha Ugavi	42,324,593.00	50,780,000.00
18.	Kitengo cha Uchaguzi	48,000,000.00	13,000,000.00
19.	Kitengo cha TAHEMA	13,400,000.00	16,050,000.00
20.	Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI	21,688,000.00	10,000,000.00

Umbile la bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017

A. Mapato

(i). Mishahara - ya Ruzuku Tshs. 20,691,872,168.00
(ii). Mapato ya Ndani Tshs. 2,317,292,200.00
(iii) Ruzuku toka serikali kuu - OC Tshs. 1,701,202.000.00
(iv) Ruzuku za maendeleo (Serikali Kuu & Wafadhili) Tshs. 6,569,028,768.00
Jumla ya mapato yote Tshs. 31,279,395,136.00

B. Matumizi

(i) Matumizi ya Mishahara - Ruzuku toka Serikali Kuu sh.20,691,872,168.00
(ii) Matumizi ya Kawaida - Ruzuku toka Serikali Kuu sh. 1,701,202,000.00
(iii) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo – Ruzuku Serikali Kuu & wafadhili shilingi 6,569,028,768.00
(iv) Matumizi ya Miradi ya Maendeleo-Mapato ya Ndani sh.1,390,375,320.00
Jumla ya matumizi yote Tshs. 31,279,395,136.00

Mkurugenzi Mtendaji (W) alitaja changamoto za jumla zinazoikabili Halmashauri kuwa ni pamoja na:-

i. Fedha toka Serikali Kuu kuchelewa kuletwa ama kuletwa kwa kiwango kidogo ukilinganisha na bajeti na wakati mwingine kutoletwa kabisa kwa matumizi ya kawaida na kwa miradi ya maendeleo
ii. Ubovu wa barabara unaosababishwa na ufinyu wa bajeti.
iii. Kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi na usafirishaji
iv. Mwamko mdogo wa baadhi ya wananchi kujitolea kuchangia miradi ya maendeleo
v. Uchache wa vitendea kazi mathalani gari kwa ajili ya ufuatiliaji wa mapato vijijini na usimamizi wa miradi
vi. Baadhi ya wafanyabiashara kutolipa ada na ushuru wa Halmashauri kwa viwango vinavyostahili.
vii. Kuwepo kwa wakandarasi wasio waaminifu ambao wanafanya kazi chini ya viwango.
viii. Kuwepo kwa sheria za manunuzi ambazo si rafiki zinazofanya gharama za manunuzi kuwa za juu (GPSA) ukilinganisha na thamani/gharama halisi ya bidhaa dukani/sokoni

Baada ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kuwasilisha mapendekezo ya mpango wa bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia na kujadili bajeti hiyo kwa kila Idara na Kitengo. Mjadala ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mhe. Kulwa D. Shoto alisema kuwa changamoto ya fedha za matumizi ya kawaida (OC) na miradi ya maendeleo kutoletwa kama ilivyo kwenye mpango wa bajeti ama kutoletwa kwa wakati au kutoletwa kabisa kwa baadhi ya miradi husababisha kushindwa kutekeleza bajeti tunayopanga. Alishauri Serikali Kuu kutekeleza wajibu wake kama ilivyo kwenye mpango wa bajeti.

Mhe. Mkomba P. Daud alisema kuna bajeti imetengwa kwa ajili ya maadhimisho mbalimbali mathalani siku ya usafi wa mazingira, wiki ya Serikali za Mitaa n.k. Alishauri fedha hiyo ipelekwe katika ununuzi wa dawa kwa ajili ya zahanati na vituo vya Afya badala ya kutumika kwa maadhimisho tu. Pia alishauri fedha zinazotengwa kwa ajili ya zawadi kwa watumishi hodari, mmoja kila Idara igawanywe kwa watumishi watano au sita kwani watumishi wa idara ni wengi.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa zawadi kwa watumishi hodari kiasi cha shilingi 500,000.00 ni maelekezo ya kisera kwa kushirikiana na vyama vya

wafanyakazi. Watumsihi wa Idara husika hupendekeza zawadi kwa watumishi hodari mmoja na kamati Tendaji ya Halmashuri huthibitisha jina hilo.
Mhe. Doa M. Limbu alitaka kujua mwaka 2015/2016 tuliidhinisha kununua mitambo ipi ya kutengeneza barabara kwani anaona kwenye bajeti hii ya 2016/2017 tunapendekeza kununua *excavator* kwa Tshs. Milioni 345.

Mkurugenzi Mtendaji (W) alifafanua kuwa Halmashauri ilishindwa kununua *excavator* na *low bed* kwa mwaka 2015/2016 kwa kuwa fedha hiyo ilielekezwa kwenye ujenzi wa maabara. Hadi sasa low bed na *tractor head* tayari limeanunuliwa na katika mwaka 2016/2017 *excavator* litanunuliwa.

Mhe. Ester I. Matone alipongeza mpango wa bajeti kwa ujumla kwani imegawa miradi ya maendeleo kwa usawa kwa kila kata. Alitaka kujua kuhusu ununuzi wa sare kwa watumishi 19 wa Idara ya Utawala wakati watumishi wa Idara hiyo ni wengi, alishauri fedha hiyo Tshs. 1,200,000.00 ielekezwe katika Kata.
Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza sare hizo siyo kwa ajili ya watumishi wote bali ni kwa ajili ya mgambo na walinzi wa Halmashauri

Mhe. Emanuel N. Makashi alisema ameona kwenye mpango wa bajeti kuna posho mbalimbali kama vile posho ya kujikimu na masaa ya ziada. Alishauri posho za masaa ya ziada zifutwe kwenye mpango wa bajeti.

Katibu Tawala (W) alieleza kuwa kifungu cha masaa ya ziada kwa watumishi ni lazima kuwepo, mathalani, waendesha mitambo ya barabara wanapokuwa vijijini wakitengeneza barabara ni lazima walipwe masaa ya ziada na posho ya siku kwani watafanya kazi hadi jioni na kulazimika kulala huko, vivyo hivyo kwa watumishi wanaposafiri nje ya Halmashauri kwa kazi mbalimbali za Serikali.

Mhe. Pili E. Sonje aliunga mkono mapendekezo ya mpango wa bajeti yaliyowasilishwa na kusema bajeti iko vizuri na imezingatia uwiano sawa wa miradi ya maendeleo kwa kila kata. Kwa kuwa hilo limezingatiwa na masuala mengine yaliyosalia yametengenezewa bajeti kwa kuzingatia uhitaji na makadirio kikomo ya bajeti, alishauri Baraza la Madiwani kupitisha bajeti hiyo kwa kauli moja.

Wajumbe waliungwa mkono rai hiyo na kupitisha mapendekezo ya mpango wa bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wenye jumla ya shilingi 31,279,395,136.00

MUHT. NA. BM/36/2015/2016 – KUFUNGA MKUTANO

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwashukuru wote walishiriki mkutano huo. Alisema kuwa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2016.2017 ni utengenezaji wa madawati ya shule za msingi, kwa sasa shilingi 5,000,000.00 ambayo ni zawadi ya ushindi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2015 zinatumika kutengeneza madawati kwa kutumia mafundi waliopo kwenye karakana iliyopo Halmashauri. Kwa sasa tatizo la uhaba wa madawati kwa shule za sekondari katika Halmashauri yetu limekwisha.

Kuhusu bajeti kwa ujumla, Mkurugenzi Mtendaji (W) alisema alijitahidi kugawa miradi ya maendeleo kwa usawa katika kila kata lakini kwa kuzingatia umuhimu wa mradi husika na vipaumbele vya Serikali.

Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha mwenyekiti kufunga mkutano.
Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa maoni na ushauri waliotoa katika bajeti hii tena kwa kuzingatia vipengele. Alisema ni wajibu wetu kupokea na kutekeleza miongoza inayotolewa na serikali na huo ndiyo uzingatiaji wa sheria na taratibu zilizopo hivyo kuondoa migongano katika utendaji. Mwenyekiti alisema kuwa Baraza la Madiwani limeridhia mapendekezo ya mpango wa bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wenye jumla ya shilingi 31,279,395,136.00

Mwenyekiti alifunga mkutano saaa 07:37 mchana

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

.....	.....	.....
Ndg. Isabela O. Chilumba	**TAREHE**	**Mhe. Juma A. Kimisha**
KATIBU		**MWENYEKITI**